**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA LONGIDO 2023

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI LONGIDO

S.L.P 8530, NAMANGA – ARUSHA
Tel +255272539218. Website: www.longidosec.sc.tz E-mail. Longido.secondary@yahoo.co.uk

**Namba za Simu-.Mkuu wa Shule: 0784-632810**

**Makamu wa Shule: 0784-168835/0786-536973**

**Matron/Patron:0682-164089**

**SHULE YA SEKONDARI LONGIDO**

**S.L.P 8530, NAMANGA -ARUSHA**

**Tarehe 13/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P ..........................................**
**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LONGIDO ILIYOPO HALMASHAURI YA LONGIDO MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari LONGIDO ipo umbali wa Kilometa 79 Kutoka Arusha mjini, Barabara ya Arusha - Namanga Usafiri kutoka mjini niwa Noah au Hiace ambao unapatikana stand kuu ya mabasi kwa Nauli ya Shilingi **6,000/=** na utashuka kituo cha polisi Longido, usafiri wa pikipiki ni Tsh 1,000 hadi shuleni.
Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**SARE YA SHULE**

Uvaaji wa sare ya shule ni lazima kwa kila mwanafunzi, hivyo mwanao awe na sare ya shule kama ifuatavyo:

**WAVULANA.**

i. Shati 2 nyeupe za mikono mifupi za aina ya tetroni na siyo mitumba.
ii. Suruali 2 rangi nyeusi, siyo mitumba, ziwe ndefu na zisizobana, ziwe na selebresheni (marinda) mbili, zenye mifuko ya pembeni kwa mshono wa "V" na mfuko wa nyuma mmoja na ziwe zimepindwa kwa chini (turn up) (Suruali zinazobana 'model' haziruhusiwi kabisa).
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2, viwe vya kufunga kwa kamba/gidamu, visivyo na kelele na visiwe vizito wala virefu kwa mbele.
iv. Soksi nyeusi fupi jozi 2.
v. Nguo za michezo: Raba, jezi rangi ya njano (yellow) (bukta na tshert)
vi. Suruali 2 za rangi ya bluu bahari (light blue) kwa ajili ya kushindia mara baada ya masomo kwa kuwa nguo za nyumbani hazirihusiwi, ziwe zimepindwa kwa chini (turn up)
vii. Sweta maruni (damu ya zee) na tai nyeusi yenye mistari meupe za darasani.
viii. Taulo moja kwa ajili ya kuogea

**WASICHANA**

i. Sketi 2 za rangi nyeusi, ziwe nzito na zenye marinda mengi, ziwe ndefu zinazofunika soksi.
ii. Shati 2 nyeupe za mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2, vya kufunga kwa kamba/gidamu (siyo simple shoes), visivyo na kelele na visiwe vizito wala virefu kwa mbele.
iv. Soksi ndefu nyeupe jozi 2
v. Nguo za michezo: Raba, jezi rangi ya njano (yellow) (bukta na tshert)
vi. Gauni 2 za rangi ya bluu bahari (light blue) zenye mikono mifupi na zenye makunjo/marinda, kwa ajili ya kushindia mara baada ya masomo kwa kuwa nguo za nyumbani haziruhusiwi.
vii. Kwa Waislamu, mfano wa Hijab iliyochaguliwa kutumika kwa wanafunzi wa kike imeambatanishwa.



viii. Sweta maruni (damu ya mzee) na tai nyeusi yenye mistari meupe za darasani.
ix. Kanga vipande viwili na taulo kwa ajili ya kuogea

**LAZIMA KWA WOTE**

Mwanao aje na yafuatayo:-

i Fomu Maalum ya kuthibitisha Afya yake (medical form) ambayo imeambatanishwa katika fomu hii, fomu hiyo ijazwe na kupigwa muhuri na daktari na iwasilishwe shuleni pindi atakapowasili. **(TATIZO SUGU LIWEKWE BAYANA)**
ii Sweta ya rangi ya bluu bahari (light blue) kwa ajili ya kushindia baada ya vipindi darasani.
iii T-sheti za bluu mbili zisizo na maandishi yoyote zenye kola na siyo shingo ya mduara kwa ajili ya kushindia baada ya vipindi darasani.
iv Picha nne za mwanafunzi za passport size awe amevaa shati nyeupe tu.
v Sanduku gumu la bati kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake kwa ajili ya usalama
vi Fedha (pocket money) kwa ajili ya matumizi yake binafsi
vii Saa ya mkononi na **tochi** isiyotumia umeme
viii File la kuweka kumbukumbu ya mitihani ya ndani na nje
ix Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
x Madaftari 12 makubwa (counter book quire 3)
xi **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
xii Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Baadhi ya *orodha imeambatanishwa*)
xiii Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
xiv Scientific Calculator kwa wanafunzi wa PCB,CBN,CBG na HGE
xv Godoro (original) lenye ujazo sahihi na lenye upana na urefu wa $2\frac{1}{2}$ x 4, lenye foronya ngumu NB; zingatia vipimo vya godoro ili viendane na vitanda vya shule.
xvi Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket moja
xvii Nguo za ndani za kutosha;
xviii Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xix Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xx Vifaa vya usafi (wavulana walete hard broom 1, sqeezer 1 na reki 1 na wasichana jembe 1, soft broom 1 na fagio za chelewa mbili).
xxi Mzazi/Mlezi hakikisha mtoto wako anakuwa na **Bima ya Afya** kwa muda wote wa masomo hapa shuleni

### 2.1 Michango mbalimbali

#### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** mchango wa uendeshaji wa shule, tahadhari na Nembo ulipwe kwenye account ya shule, **NMB 42501200023. Jina Longido secondary school.** Mwanafunzi aje na slip ya Bank yenye jina lake na Tahasusi yake siku ya kuripoti shuleni.

- Mchango wa kitambulisho cha shule mwanafunzi aje nayo mkononi

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi **haruhusiwi kubadili dini** wala **kumshawishi mwanafunzi** mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda ambacho hajapangiwa au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LONGIDO**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ........................................

**Jina la Mkuu wa Shule .DANIEL G. TEMU**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ............................................

HEADMASTER LONGIDO SECONDARY SCHOOL P. O. Box 8530 NAMANGA ARUSHA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. <u>TAFADHALI</u> UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**NB:** *Mzazi unashauriwa kumfungulia mwanao account ya Bank (NMB) ili kurahisisha utoaji na uwekaji wa fedha (pocket money) kwani huduma hizi za Bank ya NMB zinapatikana shuleni kwa ukaribu zaidi (kwa yeyote ambaye hana account ya NMB huduma hiyo inatolewa shuleni na NMB Bank kwa Tsh 10,000/=)*

- **Mkuu wa shule: 0784-632810**
- **Makamu wa Shule :0784-168835/0786-536973**
- **Mwandamizi Taaluma :0762347047**
- **Mwandamizi Malezi :0786-580292**

**SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA**

1. (i) Jina la Mwanafunzi ..............................................................................................
   NB: Jina liwe lile lililotumika katika mtihani wa Taifa kidato cha nne.
   (ii) Jina la Shule uliyomaliza elimu ya kidato cha nne ................................................
   (iii) Tarehe ya kuzaliwa ......................... kijiji ............................
   kata ...................... Tarafa .................. Wilaya .....................Mkoa .................

2. **AFYA:**
   (i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliyowahi kuugua kama vile TB, POLIO, KIFAFA, UKIMWI n.k...........................................
   (ii) Taja matatizo yoyote ya afya yako .....................................

3. JINA LA MZAZI
   (i) Baba ............................................ Hai/amefariki lini ......................................
   (ii) Mama ......................................... Hai/amefariki lini ........................................

4. KAZI YA:
   (i)Baba ............................. Dini .................... dhehebu ...........................................
   (ii)Mama ........................... Dini .................. dhehebu .......................................
   (iii)Anwani ya mzazi/mlezi ..................................................................................
   (iv) Mwanafunzi anaishi na (weka alama V sehemu iliyo sahihi)
   (a) Baba tu [ ] (b) Mama tu [ ] (c) Wazazi wote wawili [ ] (d) Mlezi [ ]

5. MZAZI/MLEZI/TAASISI ITAKAYOGHARAMIKIA MAHITAJI YA SHULE:
   (i) Jina .................................................................... (ii) Kazi yake ni
   ............................................................ (iii) Anuani ya
   mzazi/mlezi............................................
   (iv) Namba yake ya simu .................................................
   (v) Uhusiano wake........................ Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba n.k.
   (vi) Dini yake ............................ Dhehebu ................. (vii)

**NB: Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada kwa haraka na picha (passport) zao kwenye ukurasa wa kwanza wa fowm hii.**

| SN | JINA KAMILI | KAZI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

6. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:
   Mimi ...............................................Kidato cha ......... Nimezisoma na kuzielewa sheria/taratibu/kanuni zote za shule na hivyo ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Longido na ninaahidi kuwa nitafuata sheria/taratibu/kanuni zote za shule ili nitimize lengo la kuja shule kwa manufaa yangu, familia, jamii na taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na sheria/taratibu /kanuni za shule nitakubali kuadhibiwa/kufukuzwa shule.

   Saini ya Mwanfunzi .......................... Tarehe ....................

7. **SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI/TAASISI HUSIKA.**

Mimi......................................................ambaye ni ......................nathibitisha kuwa taarifa hizo hapo juu ni sahihi. Nimezisoma na kuzielewa sheria/taratibu/kanuni zote za shule na ninakubali mwanangu apewe adhabu/afukuzwe shule ikiwa atakiuka sheria/taratibu/kanuni za shule. Ninaahidi kushirikiana na Uongozi wa shule na Watumishi wote kuhakikisha mwanangu anakuwa na Nidhamu na Juhudi katika masomo, nitagharamia mahitaji yake ya shule ili kumjengea mazingira mazuri ya kusoma katika kipindi chote atakachokuwa shuleni.

Saini ya Mzazi/Mlezi ................................ Tarehe .................

**NB:** Kama mwanafunzi/mwanao ana Bima ya afya aje nayo shuleni

VITABU VYA REJEA KWA MWANAFUNZI

HISTORIA

1. Yassin.S. (2010) History Essential In Advanced Level Ahmagiyya Printing Press. Dar.Es.Salaam.

KISWAHILI

1. Masebo A.J & Nyangwine. N.(2015). Nadharia Ya Lugha Ya Kiswahili, Nyambari Publishers, Dar-Es-Salaam

KIINGEREZA

1. Nyangwine N (2015),Advanced Level English Language form 5&6. Nyamari Publisher, Dar-es-salaam

**GEOGRAPHY**

1. Kamili . Z(2021) Physical Geography, Kamili Books And General Supplies. Dar-Es-Salaam

**CHEMISTRY**

1. CHAND S.(2$^{nd}$ edition 2006) conceptual chemistry , New Delhi India.

**BIOLOGY**

1. Tailor D; Soper R.J (1999) Biological science (BS) Cambridge University UK.

**PHYSICS**

1. Chands S. Meta Rohit Mheta K. V (2006) Principle of Physics Delhi India.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## MEDICAL EXAMINATION FORM

*(To be completed by a Medical Officer in respect of both Form I and V entrants)*

Student's Full Name ……………………………………………………………………

Blood count(*red and white*) ……………………………………………………………………

Stool Examination ……………………………………………………………………

Urinalysis ……………………………………………………………………

Syphilis test ……………………………………………………………………

TB test ……………………………………………………………………

Eye test ……………………………………………………………………

Ears ……………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………
Pregnancy test (*for girls*)
……………………………………………………………………
Abdomen ……………………………………………………………………
Spleen ……………………………………………………………………
Additional information, for example Physical defects, infections, chronic or family disease etc.
……………………………………………………………………………………………………
…

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……

I certify that the student mentioned above is Normal/Bear attention to him/her for pursuing further studies.

Designation ……………………………………

Station ……………………………………

Signature and Official stamp ……………………

Date ……………………………………